

## UTARATIBU WA KULE KUNYAKULIWA KUKUU

*1Wathesa 4:13-18... Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele.....*

Na sasa, nataka kuzungumza juu ya hilo usiku huu wa leo. Na somo langu litaenda kuwa “Mambo yale yatakavyokuwa”. Na sasa, nilizungumza usiku wa jana juu ya kunyakuliwa, kwa hiyo usiku wa leo, Napenda kuzungumzia juu ya somo hili, kwamba niweze kuyafunga pamoja na ujumbe wa usiku wa jana.

Sasa, kutakuwa na kunyakuliwa; tunafahamu hilo. Hilo liko katika siku zijazo [1]

Neno “rapture” katika biblia halitumiki hata kidogo tumeliweka tu pale. Biblia ilisema, “Kunyakuliwa juu, kule kunyakuliwa juu” Tunasoma hapa katika Wathesalonike ule utaratibu wa kule kunyakuliwa kuuu ambako kutafanyika katika siku za mwisho. Sikilizeni hili hapa. Tunaenda kuanzia na mstari wa 13 “kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza”

Sasa, nataka uone jambo kubwa linalotendeka sasa usilikose hili. Angalia, kutoka mstari wa 13 mpaka 16 kuna mambo matatu ambayo lazima yatokee kabla Bwana mwenyewe hajatokea. Jambo la kwanza kutokea, angalau mwaliko, sauti, parapanda.

Mambo matatu yanatokea, Mwaliko, sauti, Tarumbeta lazima yatokee kabla ya Yesu kutokea. Sasa, Mwaliko Yesu anafanya

mambo yote matatu wakati anaposhuka ule “mwaliko”, Mwaliko ni nini? Ni ujumbe unaoanza ukihubiriwa huku na huku, mkate wa uzima ukimleta yule Bibi Arusi. Sasa Mungu ana namna ya kufanya mambo yake Naye habadilishi taratibu Yake [2]

Angalia, sasa ule uhai katika mwili ni uthibitisho ya kwamba unyakuo uko karibu unapoon kile kichwa na mwili vinakuwa mmoja na ule ukamilifu wa kipimo cha udhihirisho wake, inaonyesha kwamba mwili uko karibu, tayari kupelekewa katika kichwa.

“Mataifa yanavunjika”, Waisrael wanaamka.....unaona ninachomaanisha? Ameanza kutoa uhai ndani ya mwili wake wale aliowakombo kazi ya upatanisho imefanyika. Analeta uhai wake katika mwili katika kuthibitisha ule unyakuo [3]

Yesu alisema, “kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma” sasa angalia kwa karibu, katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kule kuja kwa mwana wa Adamu, wakati mwana wa Adamu anafunuliwa” (Luka 17:26-30) siyo tena kama kanisa, siyo tena Bibi Arusi anaitwa. Unaona? “Katika siku Mwana wa Adamu atakapofunuliwa.” Nini? Kulinganisha kanisa katika kile kichwa, kuungana, Ndoa ya Bibi Arusi.

Ule mwito wa Bwana Arusi utakuja kupitia hili, wakati Mwana wa Adamu atakuja chini na kuja katika mwili wa kibinadamu kuwaunganisha hawa wawili wawili pamoja, kanisa linapaswa liwe Neno; Yeye ni Neno na hawa wawili wanaungana pamoja, na ili kufanya hivyo, itachukuwa udhihirisho wa ufunuo wa Mwana wa Adamu siyo kiongozi wa dini unaona ninachomaanisha?

Unaona, ni Mwana wa Adamu, Yesu Kristo, atakuja chini katika umbile la kibinadamu miongoni mwetu, na atalifanya Neno lake kuwa halisi sana kiasi kwamba italiunganisha Kanisa na Yeye Mwenyewe kama mmoja, Bibi Arusi, na hapo sasa ataenda Nyumbani kwenye karamu ya Arusi. Amina.

Bibi Arusi tayari ameunganishwa; tunaenda kwenye karamu ya Arusi, sio kweye ndoa. “kisha nikaona malaika mmoja amesimama katika jua; akalia kwa sauti kuu, akiwaambia ndege wote warukao katikati ya mbingu, njooni mkutane kwa karamu ya Mungu iliyo kuu; (Ufunuo 19:17) kwa kuwa arusi ya mwanakondoo imekuja”. Lakini unyakuo ni kwenda kwenye karamu ya Arusi. Wakati Neno linapoungana na mtu hapo, na hawa wawili wanakuwa mmoja, na sasa linafanya nini tena? Linamdhihirisha Mwana wa Adamu tena, siyo kanisa la kitheolojia, vyovyote Mwana wa Adamu alivyofanya, Yeye alikuwa ni Neno, Kanisa linafanya jambo lile lile [4].

Ule unyakuo unaenda kuwa ni kusanyiko la wote walalao katika mavumbi ya dunia, hiyo ni sahihi na Mungu (1Wathesa 4:16-17). Watasema, “vema, nilifikiri unyakuo utatokea kwanza”.

“Umeshatokea tayari, na hamkujua hilo. Mmeachwa” unaona “vema, kila kitu kinaendelea....” Ndiyo, Bwana.

Ni kule kuja kwa siri, unyakuo uko hivyo, unakuja kumwiba na kwenda zake. Kama kile kitabu nilichosoma wakati ule cha “Juliet na Romeo”. Alikuwa wakati wa usiku, wakati watu walikuwa wamelala katika mambo ya dunia, na kanisa lote kwenye mambo ya dunia. Na mara kwa ghafla ule ukelele unakuja, na hao wakaenda zao mbali unaona itakuwa ni siri ya kule kunyakuliwa mbali [5].

Nitaenda kuuliza hapa kidogo sasa. Lakini simaanishi. Unaona? Kwa dakika chache, dakika chache tu; ili kwamba muwe na uhakika mmeelewa. Tazama: Wale watu waliotembea na Kristo, “kwa nini maandiko yanasema kwamba Eliya ni lazima aje kwanza? Na walikuwa ni wafuasi wa Yohana na bado hawakumjua yeye (Matayo 11: 2 – 14). Kwa nini maandiko yanasema waalimu? Unaona ninachomaanisha “Kwa nini maandiko yanasema kwamba Eliya ni lazima aje kwanza? (Marko 9:11-13) wanafunzi waliotembea na Yeye. “Kwa nini maandiko yanasema kwamba ni lazima aje kwanza kabla ya mambo haya na kutengeneza mambo yote? Alifanya hivyo kwa

watu kama nusu ya dazeni, na hao tu ndio walikuwepo unaona?.

Hao ndio wote walipaswa kulipokea hilo ndio waliokusudiwa kuliona hilo.

Yesu alisema, “yeye amekwisha kuja, na wasimtambue lakini alifanya vile tu maandiko yalisema atafanya. Aliwarudisha wao, ninyi wote, ambao mmenipokea mimi na wote walioniamini mimi. Alifanya hasa vile maandiko yalisema angelifanya. Na walimfanyia vile maandiko yalivyosema wengemfanyia. Amekwisha kuja, na hamkufahamu hilo”. Mko tayari?

Nataka niwaogopeshe kidogo unyakuo utakuwa hivyo hivyo itakuwa rahisi sana; hapana shaka itakuwa hivyo hivyo mpaka unyakuo utakapokuja moja ya siku hizi na hakuna mtu atakayejua chochote juu ya hilo.

Sasa, msiinuke juu sasa, ila jifunzeni kwa dakika tu nina uhakika wa kutosha ninafunga sasa. Unyakuo utakuwa katika hali rahisi, mpaka hukumu itakapokuja, na watamuona Mwana wa Adamu; watasema, “hatukupaswa kuwa na hili na hili..... na si ilipasa Eliya atumwe kwetu? Na sisi ingepasa kuwe na unyakuo?”

Yesu atasema, “ilishatokea na hamjui hilo” Mungu katika urahisi..... unyakuo utakuwa.....wachache sana wataenda na Bibi Arusi. Itakuwa, pengine mmoja ataondoka Jeffersonville, mtu Fulani atakuja aonekane hayupo watasema, “vema, kamwe.....”Wengineo hawatajua kutokuwepo mmoja ameondoka Georgia unaona? Kutakuwa na mmoja anaondoka katika Afrika na hebu tuseme watakuwepo watu mia tano wanaoishi wataenda katika kubadilishwa (1kor 15:51-54). Sasa, huo sio mwili wa kanisa; huyo ni Bibi Arusi Hilo siyo kanisa; huyo ni Bibi Arusi. Unaona? Kanisa litakuja juu kwa maelfu, lakini hiyo ni ule ufufuo mwingine (ufunuo20:4-6,11-15) Hawakuwa hai kwa muda wote wa miaka elfu unaona? Lakini katika Bibi Arusi kama watu mia tano wataondoka duniani katika dakika hii, dunia haitojua lolote juu ya hilo.

Yesu alisema, “kutakuwepo wawili kitandani; nitachukua mmoja nitaacha mmoja”Huo ni wakati wa usiku kutakuwepo wawili shambani (katika upande mwingine wa dunia); nitachukuwa mmoja na nitaacha mmoja. Na kama ilivyo kuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyo kuwa katika siku za kuja kwake mwana wa Adamu” (Luka 17:26-36)

Fikiria. Kila kitu kitaendelea kama kawaida iwezavyo kuwa. Mungu anazungumza na unyakuo unatokea. Siyo kwenda pale, na Malaika washuke chini na chepe kule makaburini na kutoa mzoga wa zamami uliokufa pale, ni nini? Umezaliwa katika hali ya dhambi kwa kuanzia, lakini uko mpya uliombwa kwa mfano wake. Itakuwa ni siri, kwa sababu alisema atakuja kama mwizi wakati wa usiku (Matayo 24:37-44).

Yeye amekwisha kutuambia haya, ule unyakuo, halafu hukumu zitapiga; dhambi, mapigo, magonjwa na kila kitu. Watu watalilia kifo kiwachukue wakati wa hukumu .....(Ufunuo 9:6) “Bwana, kwa nini hukumu hizi ziko juu yetu wakati ulisema kwamba kutakuwa na unyakuo kwanza?”

Naye atasema, umekwisha kuja na hamkujua hilo” Mungu akijificha mwenyewe katika urahisi oh jamani hilo ni sahihi. Tayari hilo limetokea na wewe hukujua”

Kwa nini waaminio wasiamini ishara rahisi za kuja kwake? Wanategemea mambo haya yote yaliyozungumzwa kwenye maandiko, na mwezi utakuwa giza jua katikati ya siku, na kutakuwa na mambo ya aina zote Matayo 24:29-31. [6]

Kwa hiyo, tunajua tuko wakati wa mwisho; tuko hapa sijui ni kwa umbali gani; hataacha tujue hilo, kwa sababu kuja kwake ni kama mwizi ajavyo wakati wa usiku. Lakini marafiki, ndugu zangu, dada, na tuwe tayari bila kujali. Hebu na tujiandae wenyewe unaona, kwa sababu dunia itaendelea kama kawaida. Kamwe hawatajua kama umetokea. Wakati milango ya rehema itakapofungwa, wahubiri wataendelea kuhubiri wokovu, na kuwafanya watu watubu, wataendelea mbele kama tu

ilivyokuwa siku zote. Ilifanya hivyo nyakati nyingine na itakuwa hivyo katika wakati huu. Na unyakuo utakuwa ni ghafla sana na haraka sana kiasi kwamba dunia haitakuwa imewakosa kamwe, kwamba wameondoka. Hiyo ni kweli hawatajua lolote juu ya hilo anakuja na kumuondolea bibi Arusi mbali. Itakuwa ameondoka; hawatajua chochote juu ya hilo. Kwa hiyo Ombeni, niombeeni nawaombea ninyi hatujui saa hiyo itakuwa lini, lakini tunaamini itakuwa karibuni sana. Na kaeni mbali na vitu vinavyong’aa kaeni na injili mnaona? Kaeni hapa sasa na muombe...[7].

#### Nukuu za Kiingereza

[1]mambo yale yatakavyokuwa Aya 20

[2] kule kunyakuliwa aya 128-131

[3] kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa uk 77/78

[4] kuthibitisha neno lake (64-0816) , aya 236

[5] Bwana mara moja tena (63-0628m), Aya 203-206

[6] Mungu katika urahisi kitabu cha mihuri uk 57-59

[7] aliye ndani yako Aya 25

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 160 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberge, Germany Simu (+49) 72357613 Fax (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyochaguliwa kimbele imesikia.

Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:

Charles E. Y. Kanju,  
Box 553 Korogwe - Tanga  
E-mail: Chaelika@live1.com  
Cellphone: 0784 704299/ 0718230098